1. **MPANGO WA MAENDELEO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**1.0. UTANGULIZI**.

Wilaya ya kati ina takribani ya Watu 132,717 kwa mujibu wa sensa ya 2022, Wadi nane (8) na Shehia 42. Baraza la Manispaa kati lina Jumla ya Wafanyakazi 153 kati ya hao wa kudumu 83, mkataba maalum 70. Vile vile Baraza la Manispaa Kati lina waheshimiwa Madiwani 16 (viti maalum 3, wa kuteuliwa na wananchi ni 8 na wa uteuzi wa Mhe Waziri (TAMISEM 5).

Kwa mwaka wa fedha **2026/2027**, Baraza la Manispaa kati litaendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia miongozo ya Serikali kuu , ilani ya Chama cha CCM na ahadi za viongozi wakuu wa Serikali. Pia baraza la Manispaa linalazimika kuyasimamia na kuyatekeleza majukumu yaliyotajwa katika sheria namba 7 / 2014 ya Serikali za Mitaa na Kufuata Mpango Mkakati Tuliojiwekea wa Miaka sita (6) (2024/25 -2029/30).

**1.0 MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/2027**

**2.1 Vipaumbele vya Miradi ya Maendeleo**

Kwa Mwaka wa fedha 2026/2027, Baraza la Manispaa kati limepanga kutekeleza Miradi ifuatayo kwa kuzingatia mahitaji ya Wananchi ambayo pia itakua chanzo kikubwa cha kuongezeka Mapato ya Baraza. Miradi yenyewe ni kama vile:

- Ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia Watoto (Tunguu) (chanzo cha fedha- SMZ)
- Ujenzi wa vizimba vya kutupia taka kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na mradi wa Big Z( chanzo cha fedha- mapato ya ndani)
- Maandalizi ya jengo la biashara (Tunguu Complex) ( chanzo cha fedha – mapato ya ndani).
- Maandalizi ya Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi

## 1.0 MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Bajeti ya Mwaka 2026/2027 imepangwa chini ya usimamizi wa divisheni na Vitengo vilivyopo ambavyo ni;-

1. Divisheni ya Utumishi na Utawala ikiwemo vitengo 6.
2. Divisheni ya Mapato, uchumi na Wajasiriamali
3. Divisheni ya Mazingira na Mipango miji.

Kutokana na marekebisho ya bajeti yaliyotumwa na Wizara ya fedha na mipango Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Baraza la Manispaa Kati limepangiwa kukusanya jumla ya Shilingi **2,357,287,200/**= badala ya **shilingi 1,955,000,000** ambazo zilijipangia wenyewe kukusanywa;-

Kupitia makusanyo hayo haliyoshushwa kumetolewa mgawanyo wa matumizi kama ifuatavyo:-

1. Asilimia **10** zitawasilishwa Mfuko wa kuwainua Wananchi kiuchumi (ZEEA) shilingi **235,728,720 /=.**

Fedha zilizobakia ambazo ni jumla ya shilingi **2,121,558,480** /= zitagawiwa sehemu 2 ambazo ni 50 kwa 50 kama ifuatavyo:-

2. Asilimia **50** zitumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo ni jumla ya **shilingi 1,060,779,240 /=**
3. Asilimia 50 shughuli za uendeshaji wa baraza ambazo ni shilingi **1,060,779,240 /=**

Vile vile jumla ya shilingi **1,016,830,000 /=** zinatarajiwa kuwa ruzuku ya Mishahara kwa Wafanyakazi wa kudumu wa Baraza la Manispaa Kati kutoka Serikali kuu na kufanya jumla ya bajeti yote ni **Shillingi 3,374,117,200/-**

## 2.0 Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa ukusanyaji mapato na kuimarisha miji.

Kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Baraza la Manispaa Kati limekusudia kuongeza ufanisi katika ukusanyaji mapato na kuimarisha Miji ikiwemo**:**

1. Kuendelea kubuni Vyanzo Vipya vya Mapato ikiwemo Miradi ya ujenzi wa majengo mapya ya biashara, minada ya samaki na uanzishwaji wa maegesho (Parking) katika mikusanyiko ya watu kama vile masoko.

2. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kulipa tozo za kisheria kwa hiari.
3. Kuboresha vyanzo vilivyopo ili kuongeza mapato.
4. Kufanya ziara za ukaguzi wa leseni katika maeneo mbalimbali ikiwemo Maduka, Viosk na maeneo ya Ujenzi.
5. Kupendezesha miji kwa kupanda bustani na vivutio katika mizunguko (round about) na pembezoni na katikati mwa barabara.
6. Upandaji miti katika sehemu mbali mbali zikiwemo pembezoni mwa barabara na maeneo yote yalioathirika na uchimbaji wa mchanga, kifusi au mawe.

**3.0 Usafi wa Mazingira na Kupendezesha Mji.**

a. Kuendelea Kufanya Kampeni ya Safisha, Pendezesha Wilaya ya Kati kwa lengo la kuimarisha usafi.
b. Kuendelea kuelimisha jamii juu ya suala zima la usafi wa mazingira
c. Kuendelea kutoa onyo na kutumia sheria zilizowekwa juu ya kuimarisha usafi
d. Kutunga sheria ndogo ndogo (by laws) juu ya uimarishaji wa usafi wa mazingira
e. Kusafisha maeneo ya barabara kuu na za ndani na kuondoa Majaa yasio rasmi.
f. Ununuzi wa Magari ya kuzolea taka na Vifaa vya Usafi.
g. Kushirikisha Taasisi binafsi katika suala la taka hususan katika maeneo ya Hotelini na majumbani.
h. Ununuzi wa gari la taka.

**4.0 HITIMISHO**

Mwelekeo wa bajeti na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 utafanikiwa iwapo Baraza la Manispaa Kati litafanikiwa kukusanya mapato kama lilivyojipangia. Pia na kupata ushirikiano na msaada kutoka kwa taasisi mbalimbili za ndani na nje ya Wilaya ya Kati. Kwa upande wa Baraza la Manispaa Kati limejidhatiti kuhakikisha linaongeza vyanzo vya mapato na kuanzisha miradi mipya ili kusudio la

Serikali kuu na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kuwahudumia wananchi kwa ufanisi linatafanikiwa.

**VIAMBATANISHO.**

**KIAMBATANISHO NO.1. MAKUSANYO YA MAPATO KWA VIANZIO JULAI-MACHI 2025/2026.**

**KIAMBATANISHO.2. VIKUNDI VYA WAJASIRIAMALI VILIVYOPATIWA MIKOPO JULAI - MACHI 2025/2026.**

| S/N | JINA LA KIKUNDI | SEHEMU KILIPO |
|---|---|---|
| 1 | TUJIGOMBOE COOPERATIVE SOCIETY. | PETE |
| 2 | UMOJA WETU COOPERATIVE. | NDAGAA |
| 3 | SUBIRA NI NGAO. | KITUMBA |
| 4 | ABEBWAE HUJIKAZA COOPERATIVE. | KIKUNGWI |

**KIAMBATANISHO.2 WAJASIRIAMALI WA MAHITAJI MAALUMU WALIOPATIWA MIKOPO KWA MAKUNDI MAALUMU JULAI - MACHI 2025/2026**

| S/N | IDADI YA WATU | WANAWAKE | WANAUME |
|---|---|---|---|
| 1 | 15 | 11 | 4 |

**KIAMBATANISHO: NO.3 KESI ZILIZOSIKILIZWA KUPTIA MAHAKAMA KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2025/2026.**

Kitengo cha Sheria kimeweza kusikikiliza kesi kumi na nane (18) nje ya Mahakama na kesi moja kusikilizwa Mahakamani..

| NO | AINA YA MAKOSA | IDADI YA KESI |
|---|---|---|
| **1** | Kufanya biashara bila ya kua na leseni | 6 |
| **2** | Kujenga bila ya kuwa na kibali | 1 |
| **3** | Kufanya biashara ya vileo nje ya muda | 1 |
| **4** | Kufanya biashara ya vileo bila ya kuwa na leseni | 2 |
| **6** | Uchafuzi wa Mazingira | 1 |
| **7** | Kufanya kero | 1 |
| **8** | Kukutwa na mifuko ya plastiki | 3 |
| **9** | Kusafirisha kifusi nje ya muda | 4 |

.

.